**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SEREKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBAHA**

# MTIHANI WA HALMASHAURI WA UTIMILIFU

**KIDATO CHA NNE**

**MSIMBO: 021** **KISWAHILI**

**MUDA: SAA 3: 00** **2025**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C yenye maswali kumi na moja (11).
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na B, na maswali mawili kutoka sehemu C ambapo swali la tisa (9) ni la lazima
3. Sehemu A ina alama kumi na sita (16), sehemu B ina alama hamsini na nne (54) na sehemu C ina alama thelathini (30).
4. Zingatia maelekezo ya kila sehemu na ya kila swali.
5. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani.
6. Andika Namba yako ya Mtihani katrika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

www.ujuziblog.com

## SEHEMU A (Alama 16)

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele (i) hadi (x), kisha andika herufi ya jibu hilo kwenye kijitabu chako cha kujibia.

(i) Katika neno 'umempelekea' mofimu ipi inawakilisha kauli ya kutendea?

A. Me-
B. –e-
C. –m-
D. –pelek-
E. –a

(ii) Kati ya maneno yafuatayo, neno lipi **haliundwi** kwa mbinu ya urudufishaji?

A. Polepole
B. Fifisha
C. Rukaruka
D. Barabara
E. Kichurachura

(iii) "uzuriwe" neno hili limefupishwa katika shairi ili kuleta ulinganifu wa mizani, ni mbinu ipi imetumika kufupisha neno hilo?

A. Inkisari
B. Islafu
C. Ufupisho
D. Uhulutishaji
E. Tafsida

(iv) Kila alama ya uandishi ina kazi yake katika lugha ya kiswahili. Ipi kati ya kazi zifuatazo ni kazi ya alama ya mtajo?

A. Kutenga maneno mawili yenye maana sawa
B. Kuonesha maana ya ziada katika sentensi
C. Kubainisha maneno yasiyo rasmi katika lugha
D. Hutaja maneno yaliyo katika orodha
E. Hutumika kusisitiza jambo

(v) Wasanii wanapojenga kazi zao za kifasihii hutumia kipengele kipi?

A. Mandhari
B. Mjengo wa tungo
C. Muundo
D. Mtindo
E. Wahusika

(vi) ……………… ni mtindo wa kutumia lugha katika miktadha mbalimbali

A. Simo
B. Rejesta
C. Misimu
D. Utata

(vii) Kipashio kidogo kuliko vyote katika lugha ya kiswahili ni kipi?

A. Mofimu huru
B. Kishazi
C. Mofimu
D. Kirai

(viii) Neno "papai" linaingia katika ngeli ya ……………………………

A. PA-MU-KU
B. U-ZI
C. U-YA
D. KI-VI
E. LI-YA

(ix) Kimapokeo, nomino inayojitokeza upande wa kiarifu inaitwa ………………

A. Kiima
B. Chagizo
C. Shamirisho
D. Kiarifu
E. Prediketa

(x) Hamsini, laki, kasri, na fikiri ni miongoni mwa maneno yanayothibitisha asili ya Kiswahili ni ….
A. Kiarabu
B. Krioli
C. Kibantu
D. Pijini
E. Chotara

2. Oanisha maneno mbalimbali katika Orodha A na dhana husika katika Orodha B, kisha andika herufi ya jibu sahihi katika kijitabu chako cha kujibia

| **Orodha A** | **Orodha B** |
|---|---|
| (i) Lugha inayozungumzwa na watu wenye asili ya lugha mbili tofauti | A. Lugha mama |
| (ii) Lugha ya kibantu | B. Pijini |
| (iii) Muunganiko wa lugha za makabila tofauti zenye kufanana | C. Krioli |
| (iv) Lugha iliyounganika kati ya Kiarabu na Kiswahili | D. Kiswahili |
| (v) Lugha inayotokana na ukomavu wa Pijini | E. Kiarabu |
| (vi) Lugha yenye asili moja lakini ina tofauti ndogondogo za kimatamshi, maumbo na matumizi | F. Kibantu |
| | G. Chotara |
| | H. Lahaja |

## SEHEMU B (Alama 54)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

3. (a) Upatanisho wa kisarufi ni kigezo kimojawapo kinachounda ngeli za nomino. taja ngeli zinazopatikana kwenye sentensi zifuatazo:
(i) Sufuria nzuri imenunuliwa
(ii) Mpira mkubwa mpya umetoboka
(iii) Mzazi aliyekuja leo aliitwa na mkuu wa shule
(iv) Ugonjwa wa vipere umeenea sana
(v) Kusoma kunamanufaa sana

(b) Tunga sentensi nne (4), kila moja iwe na kiambishi rejeshi (-mo-)

4. (a) Bainisha virai vivumishi vinavyojitokeza katika sentensi zifuatazo:
(i) Mtoto mdogo anasoma kitabu polepole
(ii) Mwanafunzi hodari amefaulu mtihani
(iii) Gauni jeupe lililoshonwa limechanika
(iv) Kaka mwenye duka kubwa kijijini amewasili
(v) Nyumba kubwa nyeupe imebomolewa

(b) Andika tungo nne (4) yenye vishazi tegemezi

5. (a) Kama ulivyo mti una shina, vivyo hivyo vitenzi vya kiswahili vina mashina mabalimbali, bainisha mashina ya vitenzi vilivyopo kwenye sentensi zifuatazo
(i) Mama anaimba wimbo mzuri
(ii) Mwalimu aliwaita wanafunzi wageni
(iii)Juzi hatukusomeana vitabu
(iv)Watoto wanakimbizana barabarani
(v) Wazazi wao wanalipishana gharama zote

(b) fafanua dhana zifuatazo na kisha toa mfano mmja kwa kila dhana uliyo ifafanua

i. Kamusi
ii. Utohoaji
iii. Rejesta
iv. Sentensi

6. (a) Kiswahili kilipita kwenye nadharia mbalimbali ili kutafuta asili yake. Fafanua nadharia nne (4) zinazoeleza asili ya kiswahili

(b) Pamoja na kwamba Wajerumani walisaidia kukuza na kueneza lugha ya kiswahili, yapo mambo waliyoyafanya na kupelekea Kiswahili kudumaa. Taja mambo matano (5) yaliyodumaza kiswahili enzi za Mjerumani.

7. Kwa kuzingatia taratibu za uandishi wa matangazo ,andika tangazo la kumtafuta ndugu yako w a kiume anayeitwa Vetale Mule ambaye amepotea.

8. Soma shairi lifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata

Vivutio vya nchini, hupendeza yetu macho,
Majirani watamani, kupata tulichonacho,
Tutilie maanani, kwa wanyama tuwe macho,
Wanyamapori tulinde, ujangili tokomeza.

Wanyamapori hazina, tunu yetu kuwatunza,
Kipingamizi hakuna, kwa wanyama kuwekeza,
Faida nyingi kuona, kipato kukiongeza,
Wanyamapori tulinde, ujangili tokomeza.

Wanyama ni watulivu, binadamu majangili,
Huwaua kiuovu, tena kwa njia katili,
Huendeleza uovu, kwa yetu rasilimali,
Wanyamapori tulinde, ujangili tokomeza

## Maswali

(i) Pendekeza kichwa cha habari cha shairi ulilosoma
(ii) Bainisha vina vya kati na vya mwisho vya ubeti wa kwanza
(iii) Taja jumbe mbili ulizozipata kwenye shairi ulilosoma
(iv) Mshororo wa pili wa ubeti wa tatu una mizani mingapi?
(v) Shairi ulilosoma lina kituo cha aina gani?
(vi) Mtunzi wa shairi hili ametumia muundo gani?

www.ujuziblog.com

**SEHEMU C (Alama 30)**

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka katika sehemu hii. Swali la tisa (9) ni la **lazima**

## ORODHA YA VITABU

**USHAIRI**

| | |
|---|---|
| Wasakatonge | M.S. Khatibu (DUP) |
| Malenga Wapya | TAKILUKI (DUP) |
| Mashairi ya Chekacheka | T.A.Mvungi (EP & D.LT.D) |

**RIWAYA**

| | |
|---|---|
| Takadini | Ben J. Hanson (Mbs) |
| Watoto Wa Mama N'tilie | E. Mbogo (H.P) |
| Joka La Mdimu | A.J.Safari (H.P) |

**TAMTILIYA**

| | |
|---|---|
| Orodha | Steve Reynolds (Ma) |
| Ngoswe Penzi Kitovu Cha Uzembe | E.Semzaba (Esc) |
| Kilio Chetu | Medical Aid Foundation (Tph) |

9. Msanii wa kazi ya fasihi anafananishwa na kioo kwa kuwa hutumia ujuzi wake kuelezea mambo yaliyo kwenye jamii yake, ambayo yasingeonekana vizuri bila yeye kutumia ujuzi wake. Thibitisha dai hili kwa kutumia diwani mbili (2) ulizosoma. Toa hoja tatu (3) kila diwani

10. Waandishi wa kazi za fasihi hutumia mandhari kuonesha mambo mbalimbali yaliyopo kwenye jamii. Thibitisha hoja hii, kwa kutumia riwaya mbili (2) ulizosoma.Toa hoja tatu (3) kwa kila kitabu.

11. Elimu ya jinsia ni silaha tosha katika kupambana na maisha ya kila siku ya mwanadamu. Kwa kutumia tamthiliya mbili ulizosoma onesha madhara ambayo yanaweza kuwapata watoto wasipopata elimu ya kijinsia katika jamii

www.ujuziblog.com